
GRADE 4 -YEAR 2023 TERM 1
EXAMINATION: KISWAHILI ACTIVITIES

Maswali

SEHEMU YA 1:

1. Kusikiliza na kuzungumza
   Sema umuhimu wa vifa hivi



2. Taja miezi mitatu ya mwaka,
3. Eleza umuhimu wa mazingira

SEHEMU YA 2:

1. Kusoma
   Halima ni mwanafunzi mzuri. Nyumbani kwao wana duka kubwa sana. Humo dukani wao huuza sukari, mikate, unga na mafuta. Jana kaka alinunua kilo tano za sukari na mikate mitatu. Alimpea muuzaji pesa kisha akaenda.

   Alipofika nyumabni, mama alimuuliza, "mbona hukununua mafuta?" Kaka alisema mafuta yaliuzwa kwa bei ghali sana. Halima alitwambia kuwa duka lao huwapatia faida nyingi sana.

2. Kusoma ufahamu
   Twiga hupatikana katika maeneo ya kusini mwa Afrika, pamoja na Afrika mashariki-Kenya, Uganda na Tanzania. Ndiye mnyama mrefu zaidi duniani. Urefu wake ni kati ya mita nne nukta tatu na mita tano nukta nane. Uzito wa twiga na kilo mia nane na elfu moja, mia mbili na hamsini. Aliye na uzito wa juu ni wa kiume.

   Twiga ana maisha ya takribani miaka ishirini na mitano. Chakula chake ni nyasi na majani ambayo huyafikia kwa shingo lake ndefu sana. Ulimi wa twiga unafikia urefu wa centimita arobaini na tano.

   Mtoto wa twiga azaliwapo ni mrefu kuliko mwanadamu aliyekomaa. Mtoto huyo anaweza kusimama baada ya dakika kumi. Baada ya saa kumi anaweza kukimbia kando ya wazazi wake.

   twiga ndiye alalaye kwa muda mfupi zaidi, kati ya dakika kumi na saa mbili kwa usiku. Twiga ana uwezo wa kulala huku akisimama. Yeye ni kivutio kwa watalii.